**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
**DODOMA**

01 JUNI, 2016.

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 PAMOJA NA MAKADIRIO YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17.**

## 1.0 UTANGULIZI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/16 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambayo hujumuisha Fungu 50 - Wizara ya Fedha, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha haramu; Fungu 66 - Tume ya Mipango; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 9 (1), (c) Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 kinaipa mamlaka Kamati ya Bajeti ya kupitia na kuridhia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Bunge na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sheria inaitaka Kamati ya Bajeti kufanya mashauriano na Serikali na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama *(Fungu 40)*, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(Fungu 45)* na Mfuko wa Bunge *(Fungu 42)* na baada ya mashauriano Waziri wa fedha atawasilisha Bungeni kwa ajili ya kupitishwa. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge toleo la Januari 2016 nyongeza ya Nane, Sehemu ya tatu 9 (a) inaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha unaofuata na kulishauri Bunge ipasavyo kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana mwezi Aprili, 2016 jijini Dar es Salaam na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka

wa Fedha 2015/16 pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/17.

## 2.0 MAPITIO YA UJUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2015/16, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote manane (8) iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 8,328,509,387,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 72,659,909,000** kwa ajili ya Mishahara (PE), **Shilingi 6,390,465,067,000** ni kwa ajili ya kulipia deni la Taifa na **Shilingi 844,292,763,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,021,091,648,000** ambapo fedha za ndani zilikuwa **Shilingi 370,354,448,000** na fedha za nje zilikuwa **Shilingi 650,737,200,000**. Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 145,060,000,000** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada, mishahara isiyolipwa, gawio kutokana na hisa za Serikali, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa matumizi unaonyesha kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya **Shilingi 4,984,790,506,028.08** zilipokelewa; Kati ya fedha hizo **Shilingi 74,419,273,435** zilitumika kwa ajili ya mishahara *(sawa na asilimia 102.4 ya fedha zilizoidhinishwa hii imetokana na mishahara ya wafanyakazi wa TRA kuingizwa kwenye kifungu cha mishahara cha fungu 21, ambapo awali ilikuwa chini ya kifungu cha matumizi mengineyo);* na kiasi cha **Shilingi 4,886,279,533,417** kilipokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi mengineyo *(sawa na asilimia 67.7 ya fedha iliyoidhinishwa).* Miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi 2016 ilipokea jumla ya **Shilingi 24,091,699,176** *(sawa na asilimia 2 ya fedha zote zilizoidhinishwa).* Kati ya fedha hizo **Shilingi 21,413,499,176** zilikuwa fedha za nje na **Shilingi 2,678,200,000.00** zilikuwa fedha za ndani. Aidha, Maduhuli yaliyokuwa

yamekusanywa hadi kufikia Mwezi Machi 2016, yalifikia Shilingi **129,920,000,000** sawa na asilimia 90 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango hasa ya kusimamia Sera ya Uchumi jumla; Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Umma; Kuboresha usimamizi wa ukusanyaji maduhuli katika Taasisi za Serikali Kuu na Serikali za mitaa; Kuimarisha thamani ya Shilingi kwa lengo la kuwa na sarafu imara; Kuendelea kuhakikisha uchumi unakuwa kwa kasi; na Kuongeza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Kamati imeendelea kutoa ushauri, maoni na mapendekezo mbalimbali kwa Wizara ya Fedha na Mipango yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MAFUNGU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 .

**Mheshimiwa Spika,** hotuba iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Mipango imetoa taswira halisi ya utekelezaji wa bajeti ya Mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2015/16. Kamati imefanya tathmini katika mafungu Nane yaliyo chini ya Wizara hii na kuona yapo baadhi ya mafungu ya Wizara yamepata fedha za kutosha na hivyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, yapo mafungu ambayo hayajapatiwa fedha za kutosha na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao. (Rejea Jedwali Namba 1).

**Mheshimiwa Spika,** tathmini inaonyesha hadi kufikia mwezi Machi 2016, **Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango** lilipokea jumla ya Shilingi **48,496,535,452** sawa na asilimia 11.41 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 21 - Hazina** lilipokea jumla ya Shilingi **189,346,624,336** sawa na asilimia 15.20 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 22 - Deni la Taifa** lilipokea jumla ya Shilingi **4,651,741,834,652.08** sawa na asilimia 72.79 ya Bajeti iliyoidhinishwa; **Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali** lilipokea jumla ya Shilingi **76,250,462,743** sawa na asilimia 95.52 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina** lilipokea jumla ya Shilingi **14,196,328,053** sawa na asilimia 8.06 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 13 - Kitengo cha Udhibiti wa Fedha**

**Haramu** lilipokea jumla ya Shilingi **481,289,614** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 49.91 ya fedha zilizoidhinishwa na hakukuwa na fedha zozote za maendeleo zilizotolewa kwa fungu hili. Pia, **Fungu 66 – Tume ya Mipango** lilipokea jumla ya Shilingi **3,618,995,527** sawa na asilimia 42.25 ya fedha zilizoidhinishwa; **Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha** lilipokea jumla ya Shilingi **658,435,651** sawa na asilimia 35.92 ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango unatia shaka ukizingatia kwamba kati ya mafungu nane (8), ni mafungu mawili (2) tu *(Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali)* ndio yaliyopokea zaidi ya asilimia 70 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hadi kufikia mwezi Machi 2016. Mafungu mengine sita yamepokea fedha chini ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa, hivyo ni dhahiri kwamba utekelezaji wa shughuli nyingi za Wizara umeathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa kuzingatia mgawanyo wa majukumu na wajibu wa Serikali *(Government Instrument of 2016),* Wizara hii ina jukumu la kusimamia Sera ya Fedha *(Monetary Policy)* na Mapato na Matumizi *(Fiscal Policy)* pamoja na kusimamia Kanuni na Taratibu za Fedha nchini. Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa utolewaji wa fedha uliopo ndani ya mafungu ya Wizara ya Fedha hautoi tija kwa mafungu haya kutekeleza majukumu yao ya msingi kwa mujibu wa sheria. Mfano mzuri tunauona kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi Mkuu wa Mashirika ya Umma imepokea asilimia 8 tu ya Bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge. Hapa Kamati inajiuliza kwa kiasi hiki cha fedha ofisi hii itatimizaje malengo yake? Hali kadhalika sura hii tunaiona kwa Fungu 10, 13, 21 na 66. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango ijitathmini na kujitambua kuwa ndio Wizara Mama inatakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuhakikisha inasimamia na kutekeleza majukumu yake ya msingi hasa katika kutoa fedha kwa mafungu yake na mengine. Endapo mwenendo wa utoaji fedha utabaki kama ilivyo utaathiri kwa kiasi kikubwa utendaji kazi wa mafungu mengine.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17.

### 4.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango katika Mwaka wa Fedha 2016/17 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 9,383,606,520,094** kwa mafungu yote nane. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,583,704,480** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 8,640,242,740,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Taifa Shilingi **8,000,000,471,000** na matumizi ya kawaida **Shilingi 640,242,269,000** na **Shilingi 711,780,075,614** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 659,650,000,000 na** fedha za nje **ni Shilingi 52,130,075,614.** Aidha, Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 449,699,727,509** kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za minada na mishahara isiyolipwa, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma*.* Mchanganuo wa Maombi ya Fedha umeanishwa katika Jedwali Na.2

**Jedwali Namba 2: Maombi ya Fedha kwa Mafungu Mbalimbali yaliyoko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2016/17.**

| Na. | FUNGU | MISHAHARA | OC | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Fungu 50 Wizara ya Fedha na Mipango | 6,984,801,480 | 43,676,411,000 | 26,000,000,000 | **76,661,212,480** |
| 2. | Fungu 21 Hazina | 4,474,752,000 | 396,461,294,000 | 672,248,446,614 | 1,073,184,492,614 |
| 3. | Fungu 22 Deni la Taifa | 9,340,716,000 | 8,000,000,471,000 | - | 8,009,341,187,000 |
| 4. | Fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali | 6,784,116,000 | 38,801,749,000 | 4,869,465,000 | 50,455,330,000 |
| 5. | Fungu 7 Ofisi ya Msajili Wa Hazina | 1,974,355,000 | 158,206,645,000 | 3,458,680,000 | **163,639,680,000** |
| 6. | Fungu 13 Kitengo Cha Udhibiti wa Fedha Haramu | Inapitia Fungu 50 na Wizara nyingine | 1,103,081,000 | Hawana Fedha za Maendeleo | **1,103,081,000** |
| 7. | Fungu 66 Tume Ya Mipango | 1,560,492,000 | 1,583,291,000 | 5,203,484,000 | 8,347,267,000 |
| 8. | Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha | 464,472,000 | 409,798,000 | | **874,270,000** |
| | **Jumla** | **31,583,704,480** | **8,640,242,740,000** | **711,780,075,614** | **9,383,606,520,094** |

***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango***

## 4.2 Majukumu ya Msingi yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Waziri wa Fedha na Mipango katika hotuba yake ameeleza kwa kina majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hata hivyo, Kamati ya Bajeti bado inasisitiza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inasimamia kikamilifu tatizo la mianya ya uvujaji wa mapato na ukwepaji wa kodi; ukusanyaji hafifu wa maduhuli; kuongezeka kwa Deni la Taifa pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi. Aidha, Wizara iendelee kusimamia Sheria ya Bajeti ili kuhakikisha Bajeti zinazopitishwa na Bunge zinatekelezwa kama ziliyoidhinishwa pamoja; na kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na uwajibikaji.

# 5.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MIFUKO YA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI, MAHAKAMA NA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kwamba utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama na Bunge kuwasilishwa katika utekelezaji wa Bajeti za Sekta husika, Kamati imeona ni vyema ikatoa picha ya utekelezaji wa Bajeti za mifuko yote mitatu ili kutoa picha ya utekelezaji kabla ya kuwasilisha maombi.

## 5.1. Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi:

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi uliidhinishiwa jumla ya Shilingi **82,819,486,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 14,209,421,000** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 57,942,949,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 10,667,116,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia machi 2016, Ofisi ya Taifa Ukaguzi ilikuwa imepokea **Shilingi 37,484,851,182** sawa na asilimia 45.3 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,059,558,216** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 25,608,736,000** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,816,556,966** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo

ambapo ni fedha zote za nje. Aidha, Ofisi hiyo kwa mwaka 2015/16 ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,638,120,000** hadi kufikia Machi 2016, ilikusanya **Shilingi 7,374,747,484** sawa na asilimia 85.4 ya matarajio kwa mwaka 2015/16.

### 5.2. Mfuko wa Mahakama.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Mahakama uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 150,241,280,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 86,435,367,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Shilingi 51,485,099,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 12,320,814,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo . Hadi kufikia machi 2016, Mfuko wa Mahakama ulipokea jumla ya **Shilingi 91,682,915,307** sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 35,543,784,998** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 43,839,130,376** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 12,300,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo ni fedha zote ni za ndani.

### 5.3. Mfuko wa Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 173,768,567,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 19,413,630,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 147,354,937,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 7,000,000,000** miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia machi 2016, Mfuko wa Bunge **Shilingi 86,257,667,730** sawa na asilimia 49.6 ya bajeti iliyoidhinishiwa, kati ya fedha hizo **Shilingi 10,934,893,610** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 68,322,774,120** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 7,000,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ambapo ni fedha zote ni za ndani.

**Jedwali Na. 3 Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mahakama na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2015/16**

| MFUKO | FEDHA ZILIZO IDHINISHWA | FEDHA ZILIZOPOKELEWA HADI MWEZI MACHI | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali** | 82,819,486,000 | 37,484,851,182 | 45.3% |
| **Mahakama** | 150,241,280,000 | 91,682,915,307 | 61% |
| **Bunge** | 173,768,567,000 | 86,257,667,730 | 49.6% |

***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango***

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MFUKO WA MAHAKAMA, MFUKO WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT) NA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ya Bunge ya Bajeti ilijadili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Watendaji Wakuu wa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) pamoja na Mfuko wa Bunge kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko tajwa iliwasilisha kwenye Kamati mapendekezo ya awali kuhusu bajeti zao yaliyozingatia uzoefu wa miaka mingi katika uendeshaji wa Taasisi hizo pamoja na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi husika. Kufuatia azma ya Serikali ya kupunguza asilimia 60 ya bajeti ya matumizi mengineyo (OC) ya Mafungu yote ili fedha hizo ziende kwenye miradi ya maendeleo, hatua hiyo ilisababisha Mifuko hiyo kupewa Ukomo wa Bajeti mdogo ikilinganishwa na fedha halisi zilizoombwa na Mifuko husika. Kamati ya Bajeti iliona hili na kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko husika na kwa kuzingatia mahitaji ya msingi ya Mifuko na kukubaliana Mifuko hii izingatie ukomo wa Bajeti iliyotolewa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza bado kuna umuhimu wa kuhakikisha Mifuko husika inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kuendeshwa kwa ufanisi na tija kama Kifungu cha 23(4) cha Sheria ya Bajeti (2015) kinavyoelekeza. Kamati itahakikisha inafanya mapitio ya nusu mwaka ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 (Mid Year Review) kama ilivyo elekezwa kwenye Sheria ya Bajeti kifungu 9 (1) kipengele (h) ikiwa pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko hii kwa kipindi cha nusu mwaka na hatimaye kulishauri Bunge ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inaliomba Bunge lako liidhinishe makadirio ya Bajeti ya Mifuko hiyo kwa mwaka 2016/17 kama ilivyoanishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Namba 4: Fedha iliyoidhinishwa kwa Mfuko wa Mahakama, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT).**

| **MAKADIRIO YA BAJETI YA MIFUKO KWA MWAKA 2016/17** | | **MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40)** | **MFUKO WA BUNGE (FUNGU 42)** | **MFUKO WA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI (NAOT) (FUNGU 45)** |
|---|---|---|---|---|
| **Bajeti iliyopitishwa** | PE | 50,345,775,000 | 23,798,609,000 | 13,874,793,000 |
| | OC | 34,519,534,000 | 68,267,508,000 | 18,498,303,000 |
| | DEV | 46,761,734,000 | 7,000,000,000 | 12,285,427,368 |
| **Jumla ya Bajeti (OC, Mishahara na Maendeleo)** | | **131,627,043,000** | **99,066,117,000** | **44,658,523,368** |

***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango***

**Mheshimiwa Spika,** hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako tukufu lilidhie maombi **Shilingi 131,627,043,000** kwa ajili ya **Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**; **Shilingi 99,066,117,000** kwa ajili ya **Fungu 42 – Mfuko wa Bunge; na Shilingi 44,658,523,368** kwa ajili ya **Fungu 45 – Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**; ili kufanikisha utekelezaji wa m ajukumu ya Mifuko hiyo kiufanisi na kuleta tija inayokusudiwa

## 7.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2015/16 pamoja na maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/17; Kamati inapenda kutoa maoni na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

### 7.1.1 Mwenendo wa Utolewaji wa Fedha kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko kama ilivyo idhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya tathmini ya ujumla ya mwenendo wa utolewaji wa fedha za utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa mafungu yaliyochini ya Wizara ya Fedha na kuona haukuwa wa kuridhisha. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Kati ya mafungu Nane (8) ya Wizara hii na Mifuko Mitatu (3) ni mafungu mawili tu (Fungu 22-Deni la Taifa na Fungu 23-Mhasibu Mkuu wa Serikali) yamepata fedha zaidi ya asilimia 70 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/16. Kwa mwenendo huu inaonyesha kuwa jukumu la Wizara ya Fedha ambaye ndiye msimamizi na mtoaji wa fedha kwa Wizara nyingine litakuwa limeathirika kwa kiwango kikubwa na hivyo kupelekea kushindwa kutekeleza jukumu hili kwa Wizara nyingine. Katika kudhihirisha hili, mfano mzuri tunauona kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwamba; Kati ya mafungu 62 ya Serikali Kuu, mafungu 33 yamebainika kupewa asilimia chini ya 50, mafungu 26 yamepewa zaidi ya asilimia 50 na mafungu 3 yamepewa zaidi ya asilimia 100 ya fedha zote za matumizi mengineyo kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kamati inataka Wizara ya Fedha na Mipango izingatie majukumu ya mafungu yake sambamba na kutoa fedha iliyobakia kwa mafungu yake kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili yaweze kusimamia utekelezaji wa kibajeti kwa mafungu mengine ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

### 7.1.2 Usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jukumu la Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni kusimamia Sheria ya fedha ya mwaka 2001 (PFA) na utayarishaji wa na usimamizi wa Hesabu za Serikali. Pia inatambua juhudi za Idara hii katika kuboresha mifumo mbalimbali ya malipo ya kielektroniki yenye viwango vya kimataifa vya uhasibu kama vile *EPICOR-IFMs* na *TISS*, pamoja na uboreshaji wa utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa *(IPSAS Accrual).* Hatua hizi, zimewezesha kuimarisha usimamizi wa Fedha za Umma. Hata hivyo Kamati inaona bado kuna changamoto kubwa zifuatazo ambazo Serikali inabidi izifanyie kazi haraka ili kuongeza ubora wa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Fedha za umma:

i. Kuharakisha usambazaji wa Mkongo wa Taifa ili kupata mawasiliano ya kimtandao *(internet)* kwa Wizara, Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi wa malipo kwa wakati;
ii. Serikali ihakikishe ina haulisha mifumo mbalimbali ya taarifa za watumishi pamoja na mapato na matumizi ya Serikali kwa ufanisi. Mfano kanzi data ya *LAWSON* hauingiliani na mfumo wa *IFMS*;
iii. Serikali ihakikishe inaongeza ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya ukusanyaji kila mwaka na hatimaye kuondokana na utaratibu wa '*Cash Budget'* na kwenda kwenye utaratibu wa '*Accrual Budget*';
iv. Kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaboresha utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa *(IPSAS Accrual)* ili kuboresha uwazi zaidi katika mapato na matumizi ya Fedha za Umma;
v. Kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za umma.

### 7.1.3 Usimamizi wa Mashirika ya Umma na Soko la Mitaji

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la Kusimamia uwekezaji wa Serikali katika Mitaji ya Mashirika na Taasisi za Umma na makampuni Binafsi. Kamati

inaipongeza hatua ya Serikali kutenga kiasi cha Shilingi 169,017,000,000 kwa mwaka 2015/16; kwa ajili ya kulipia madeni na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji. Pamoja na hatua hii nzuri, hadi kufikia mwezi Machi 2016, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi bilioni 10.038 tu. Kamati inatambua ufinyu wa Bajeti uliopo hata hivyo ni vema Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ikawa inajipanga katika kukamilisha vipaumbele vyake. Uimarishaji na usimamizi mzuri wa mashirika ya umma kama yale ya ATCL, TTCL, TRL na mengine utatoa fursa ya upatikanaji wa mapato yatakayosaidia Serikali kugharamia kikamilifu Bajeti yake.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi ya Msajili wa hazina ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 342,530,000,000 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasio ya kodi. Kati ya fedha hizo Shilingi 142,530,000,000 zinatokana na Gawio, Michango ya asilimia 15 na Makusanyo ya mapato yatokanayo na makusanyo ya Mtambo wa udhibiti wa Mawasiliano unaojulikana kama *Telecommunication Traffic Monitoring Systems (TTMS)* na Shilingi 200,000,000,000 zitatokana na mauzo ya hisa zake asilimia 4 kutoka Kampuni ya Bia (TBL) na asilimia 2.5 katika kampuni ya sigara (TCC). Hadi mwezi Februari, 2016 Ofisi ya msajili ilikuwa imekusanya shilingi 344,470,000,000 sawa na asilimia 114.78 ya makusanyo yote. Pamoja na nia njema ya Serikali kuuza hisa zake katika makampuni hayo ili kuchangamsha soko la hisa na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi bado kuna haja ya Serikali kuendelea kuwekeza kwenye makampuni mbalimbali kama vile makampuni ya gesi na madini ili kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na zoezi la kufanya uperembaji na ufuatiliaji kwa Mashirika na Makampuni yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuangalia endapo yanafanya kazi iliyokusudiwa. Kamati inaona kuwa, hatua hii itawezesha kuyarudisha Serikalini mashirika ambayo yamekiuka masharti ya kimkataba. Hivyo basi, inashauri Serikali kuwa makini inapotekeleza jambo hili kwa kuzingatia Sheria na Mikataba ambayo Serikali iliingia wakati wa uuzaji, kinyume na hapo tunaweza kuliingiza Taifa katika hasara kubwa kwa kuwalipa

wawekezaji ambao mikataba yao itavunjwa bila kufuata taratibu husika. Aidha, zoezi hili likamilike haraka iwezekanavyo ili kutimiza malengo ambayo Serikali imekusudia katika kutekeleza suala hili.

***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, kwa upande wa Soko la Mitaji; Tanzania imekwisha chukua hatua za awali za kufungua soko la mitaji Tanzania *(Liberalization of Capital Market).* Inaeleweka kwamba umiliki wa hisa ni aina moja wapo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mataifa mbalimbali duniani. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza juhudi za makusudi za kuboresha mazingira ya mfumo wa Soko la Mitaji ili liweze kukidhi mahitaji ya Watanzania. Muda umefika sasa kwa Mamlaka ya Soko la Mitaji *(Capital Market and Securities Authority)* kuanza kuhakikisha makampuni makubwa ya ndani na nje yanawekeza kwenye Soko la Mitaji la hapa nchini (DSE) ikiwa pamoja na kuhamasisha kuuza baadhi ya hisa zao kwa Watanzania. Hatua hii ni muhimu sana katika kuwawezesha Watanzania kumiliki uchumi wao na kuwezeshwa kiuchumi.

### 7.2 Ulipaji wa madeni ya Mifuko ya jamii

**Mheshimiwa Spika,** moja ya eneo ambalo Serikali ina changamoto kubwa ya kulitatua ni eneo linalohusu madeni ya mifuko ya jamii ambayo kwa pamoja yanaidai Serikali zaidi ya shilingi trilioni sita (6). Pamoja na kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ilionyesha nia njema (*commitment*) ya kulipa madeni haya likiwemo lile kubwa la PSPF, bado utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua. Mfano katika mwaka wa Fedha 2015/16, Serikali iliahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni 150 pamoja na kutoa *Non Cash Bond* ya kiasi cha shilingi trilioni 2.6 ili kulipia deni la PSPF. Hadi sasa ni shilingi bilioni 83 tu zilizotolewa na hakuna *Non Cash Bond* yoyote iliyotolewa. Kamati inaona kuwa madeni haya ni tishio kubwa linaloathiri utekelezaji wa majukumu ya mifuko husika hasa la ulipaji wa pensheni ya wastaafu wanaongezeka kila mwaka. Pamoja ya kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2016/17, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 157 kulipa malimbikizo ya deni hilo; Kamati inaitaka Serikali kuongeza kasi ya ulipaji madeni ya

Mifuko ya Jamii pamoja na kutimiza ahadi yake ya kutoa *Non Cash Bond* ya trilioni 2.6 kwa Mfuko wa PSPF ili uweze kupunguza mzigo mkubwa wa malipo ya wastaafu.

### 7.3 Mradi wa *Village Empowerment* maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. (Fungu 21)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Village Empowerment maarufu kama Milioni 50 kwa kila Kijiji. Mradi huu unalenga *"Kutenga Kiasi cha Milioni 50 kwa Kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Ujasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika"*. **Kamati imebaini kwamba,** Tanzania bara ina jumla ya vijiji 19,600 ambavyo vinahitaji jumla ya Shilingi 980,000,000,000 ili kila kijiji kipewe Shilingi milioni 50. Fedha iliyotengwa chini ya Fungu 21 - Idara ya Bajeti ya Serikali chini ya mradi uitwao "Village Empowernment" ni Shilingi 59,500,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 6 tu ya fedha zote zinazohitajika, inaweza kuhudumia vijiji 1,190.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa suala hili ni mradi wa maendeleo na linahitajika kutekelezeka ndani ya miaka mitano; Kamati ya Bajeti inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

**Kwanza**, kuongeza fedha hizi mpaka kufikia Shilingi 196,000,000,000 sawa na asilimia 20 ya fedha zote zinazohitajika ili mradi ukamilike ndani ya miaka mitano;

**Pili**, kufanya utafiti wa kutosha kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi *(National Economic Empowernment Council),* ambao ndio wasimamizi wa uwezeshaji huu ili kuwandaa wananchi katika vijiji na kuhakiki utendaji na ufanisi wa SACCOS na Ushirika katika utoaji wa Mikopo.

**Tatu**, Wakati taratibu za ukamilishaji utoaji wa mikopo hii zikiendelea fedha za mradi huu ziwekwe katika Benki ya Kilimo na kuandaa dirisha maalumu litakaloshughulikia mikopo hii. Aidha, utaratibu wa utoaji wa Mikopo hii uwe shirikishi katika ngazi zote za kiutawala.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa angalizo hili ili kuepuka mradi huu kutofikia malengo yake kama ilivyokuwa kwa ***"Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kukuza Ajira*"** - maarufu kama Mabilioni ya JK; ambao wajanja wachache wasiostahili walifaidika na kuwaacha vijana wakilalamikia utaratibu uliotumika kukopesha fedha hizo.

### 7.4 Watumishi hewa

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya maeneo yaliyosababisha Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha fedha ni uwepo wa Watumishi hewa. Kulingana na taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Rais siku ya wafanyakazi tarehe 1 Mei, 2016 ni kwamba Serikali imebaini watumishi hewa 10,295, kati ya hao watumishi 8,373 wanatoka Serikali za mitaa na Watumishi 1,922 wanatoka Serikali kuu. Watumishi hao wamekuwa wakilipwa Shilingi 11,603,273,799.41 kwa mwezi na shilingi 696,196,427,964.60 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Kamati inaamini suala la watumishi hewa na mishahara hewa ni suala lenye mtandao mpana kuanzia wakati wa kuajiri, kuingiza majina hewa kwenye mfumo na utaratibu mzima wa kufanya malipo ya mishahara na wanaochukua mishahara hiyo washiriki wao. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kufuatilia mtandao huo na kuwawajibisha watumishi wote wasio waaminifu watakaobainika kuhusika katika suala hili.

### 7.5 Matumizi ya Mashine za Kielektroniki katika Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, moja ya changamoto kubwa iliyojitokeza katika ukusanyaji wa maduhuli ni baadhi ya Taasisi, wakala na Mashirika ya Umma kutotumia Mashine za kielectroniki *(EFDs)* katika ukusanyaji wa maduhuli. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zinatumia mashine za Ki-eletroniki katika ukusanyaji wa maduhuli ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato kama inavyohamasishwa kwa Sekta Binafsi nchini kutumia mashine hizo. Hivyo,

Wizara, Idara na Taasisi yoyote itakayoshindwa kutekeleza agizo hili ichukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania iliagizwa kununua mashine za EFD na kuzigawa bure kwa wafanyabiashara wanaostahili bure. Hadi sasa mamlaka imekwisha nunua mashine za EFDs 5000 ambazo ni sawa na asilimia 2.5 ya mahitaji ya mashine za EFDs 200,000 zinazohitajika nchi nzima kwa wafanyabiashara walioandikishwa. Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba kila mfanyabiashara anaestahili kutumia mashine hizo anapewa na kuanza kuitumia kabla ya ifikapo mwaka 2018 ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kusisitiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza juhudi ya kukusanya mapato zaidi, ni vyema Serikali ikaboresha mazingira yao ya kufanya kazi kwani Kamati imebaini kuwa Makamishna wa Taasisi hii ukimuondoa Kamishna Mkuu bado wanakaimu katika nafasi zao. Hii inapunguza motisha wa kufanya kazi hasa ukizngatia hawajathibitishwa katika nafasi hizo. Kamati inaishauri Serikali kuwathibitisha wale ambao wameonyesha uwezo wa kuzimudu nafasi zao na kuwaondoa wale ambao wameshindwa kutekelezwa kutekeleza majukumu yao na kuwateuwa wale ambao wanastahili.

### 7.6 Maduhuli yasiyorejeshwa na Mawakala na yasiopelekwa Benki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Agizo Na. 110 la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997 imeainisha kuwa, makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watunza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama. Aidha, Agizo la 38 (3) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakozoamua kutumia wakala kukusanya mapato, zimtake wakala huyo kuweka amana sawa na malipo ya miezi mitatu, dhamana ya benki au aina yeyote ya dhamana ambayo Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaona inafaa. Maagizo hayo yamekuwa hayatekelezwi kikamilifu na hivyo mawakala kukusanya Fedha na

kutoziwasilisha kwenye Halmashauri husika. Kwa mujibu wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kati ya mwaka 2010 - 2015 Serikali imepoteza jumla ya **Shilingi 19,352,218,982**. Upotevu huu umetokana na Serikali kutosimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa chini ya utaratibu uliowekwa kisheria. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuimarisha na kusimamia mfumo na nidhamu ya makusanyo ya fedha kwa Mamlaka za Serikali za kama ilivyoidhinishwa Mitaa ili kuepusha upotevu wa mapato kwa mawakala wasio waaminifu.

### 7.7 Ufuatialiaji na Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa, Tume ya Mipango ndiye Msimamizi Mkuu wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Tume hii imetengewa kiasi cha takribani Shilingi milioni 141 tu kwa ajili ya shughuli zote za kusafiri ndani ya nchi kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Mafungu mengine ya Wizara, Idara na Taasisi hayana fedha kabisa za kufanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kupunguza matumizi yasio ya lazima ili kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo kwa asilimia 40; Kamati inaona kuwa bila kutengwa fedha za kutosha kwajili ya usimamizi na ufuatiliaji, miradi mingi haitaweza kukamilika. Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha ya usimamizi na ufuatiliaji kwa Fungu 66 – Tume ya Mipango ili kuhakikisha malengo ya miradi ya maendeleo yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

### 7.8 Tatizo la Takwimu Sahihi za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** kuwepo kwa takwimu sahihi katika kutoa taarifa zinazohitajika ni muhimu katika kuwezesha taarifa hizo kutumiwa pale inapobidi. Kamati imebaini uwepo wa tatizo la Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kutoa takwimu zinazotofautiana juu ya suala moja. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuweka utaratibu mahususi wa kuzingatia inaitumia ipasavyo Tume ya Taifa ya Takwimu *(National Bureau of Statistics)* katika kutoa taarifa zenye takwimu sahihi kwa kuwa ndiyo yenye jukumu

la kuandaa kanzi data *(Data Base)* ya Serikali kwa ajili ya matumizi ya umma. Aidha, bado kuna umuhimu mkubwa wa takwimu zote za masuala ya fedha kuhakikiwa na kuoanishwa na Hazina kabla ya kuziweka wazi kwa ajili ya matumizi ya umma.

### 7.9 Uhakiki wa Madeni ya Watumishi na Watoa Huduma

**Mheshimiwa Spika**, Suala la madeni ya watumishi, wakandarasi na wazabuni limekuwa ni tatizo la muda mrefu na kuisababishia Serikali hasara kwa sababu kila mwaka mpya wa fedha Wizara, Idara na Taasisi hubeba mzigo wa madeni ya mwaka wa fedha uliopita. Aidha, Serikali imeonyesha nia ya kuhakikisha inalipa madeni ya watumishi na watoa huduma kupitia Wizara ya Fedha. Pamoja na hatua hii nzuri, Kamati inaendelea kushauri kuwa zoezi la uhakiki lizingatiwe ipasavyo kabla madeni hayo hayajalipwa.

### 7.10 Udhibiti wa utakasishaji wa Fedha Haramu.

**Mheshimiwa Spika,** Kitengo cha Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu kinatekeleza na kusimamia Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu ya mwaka 2006, sura ya 423 na Sheria ya udhibiti wa utakatishaji wa Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar ya mwaka 2010. Kamati imebaini kwa mwaka 2015/16, kitengo hiki kimepokea asilimia 44.68 tu ya fedha ya Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa na Bunge na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Hivyo, Kamati inasisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kitengo hiki kinaimarishwa na kupewa fedha za kutosha ili kiweze kuimarisha mfumo wa udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu unaokidhi viwango vya kimataifa utakao imarisha mfumo wa fedha na kudumisha haki na amani kwa jamii, kuleta utulivu wa kisiasa na kukua kwa uchumi endelevu.

## 8.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
16. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
17. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
18. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
19. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
20. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
21. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
22. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb

Aidha, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Philip Mpango Mb, Naibu Waziri Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Bajeti pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Lina Kitosi, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo pamoja na Sekretarieti ya Kamati Ndg. Michael Kadebe (Kiongozi), Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel F Rhobi, Ndg. Ruva Tunze, Ndg. Maombi Kakozi, Ndg. Lilian Masabala, na Ndg. Wilson E Machaine kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Josephat Sinkamba Kandege (Mb)

**kny: MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

1 Juni, 2016